

MALALAMIKO 29774 YASHUGHULIKIWA NA TUME YA UTUMISHI WA UMMA.

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Ndugu, Msomaji Ijumaa ya wiki iliyopita tulipata fursa ya kusoma Makala iliyoelezea jinsi Tume ya Utumishi wa Umma ilivyofanikiwa katika Utekelezaji wa jukumu la ukaguzi katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na 2006/2007 ambapo Mamlaka za Ajira na Nidhamu 90 zimekaguliwa. Mamlaka hizo ni Wizara 23, Idara 6, Mikoja 21 na Mamlaka ya Serikali za Mitaa 40. Aidha katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kukagua Mamlaka za Ajira na Nidhamu 74 ambazo ni Halmashauri 69 na Idara 5 za Serikali Zinazojitegemea. Pamoja na hayo katika makala ya leo tutapata fursa ya kuangalia malalamiko yaliyoshughulikiwa na Tume katika kipindi cha 2005/2006 na 2006/2007. Katika kipindi hicho jumla malalamiko 29774 yalishughulikiwa .

2.0 Mfumo wa kushughulikia malalamiko

Katika Mpango wa kimkakati wa mwaka 2005/2008, Tume ya Utumishi wa Umma imejiweka mfumo wa kushughulikia malalamiko kwa lengo la kuboresha Utumishi wa Umma na kuimarisha Utawala bora. Mfumo unaotumiwa na Tume wa kutoa malalamiko ni ule wa kuandika barua na kuituma kwa njia ya Posta, Fax, kupiga simu, kuandika barua pepe au mtumishi kufika yeye mwenyewe katika Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Umma Makao Makuu, Dar es Salaam, Mikoani na Wilayani. Aidha, Tume ya Utumishi inashughulikia malalamiko kwa njia ya maonyesho. Utaratibu huu unamwezesha

mtumishi au watumishi kutoa malalamiko yao ya kiutumishi. Kupitia utaratibu huu Tume imepokea na kushughulikia malalamiko 29774. Malalamiko hayo yametoka kwa watumishi wa sekta na kada mbali mbali za watumishi. Sekta hizo ni Wizara, Idara ya Utumishi wa Walimu na Serikali za Mitaa. Kada zilizowasilisha malalamiko ni kada za Walimu, Maafisa Watendaji wa Kata, Wanasheria, Maafisa Mifugo, Wakaguzi wa Ndani, Afisa Ardhi, Wahasibu na Wakurugenzi. Watumishi hao walilalamika kwa madai kuwa hawakutendwa haki, hawakuridhika na maslahi au maamuzi ambayo hayakuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa Mujibu wa Sheria na Kanuni ili kutenda haki na hatimaye kuboresha Utumishi wa Umma. Baadhi ya malalamiko yaliyopokelewa ni ya kawaida na mengine ni ya watumishi kutofahamu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi ambapo wahusika walielekezwa njia sahihi za kufuata ili kupata ufumbuzi wa malalamiko yao.

4.0 HITIMISHO.

Mtumishi au watumishi hulalamika kutokana na kutotendewa haki au kutoridhishwa na maamuzi au kwa kutofahamu Sheria, Kanuni na Taratibu zake. Mamlaka za Ajira zinapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zake katika uendeshaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu. Aidha, watumishi nao wanapaswa pia kuzingatia Sheria na kuchukua juhudi za kusoma na kuelewa Sheria hizo.

Ndugu, Msomaji iwapo una maoni au maswali au malalamiko tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo:

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

SIMU: 022 – 2126811 – 4.